

Maswali

1. Jina la huo mji uliitwa nani?
2. Mbona Waisraeli hawakutakiwa waingie huko?
3. Mungu aliwambia Waisraeli wafanye nini?
4. Makuhani walikuwa wangapi? Tarumbeta zilikuwa ngapi? Ilikuwa siku ngapi?
5. Kelele gani ilisikika?
6. Siku ya saba ilikuwa tofauti namna gani?
7. Mara ya saba ilipokwisha walifanya nini?
8. Nini ilifanyika baadaye?
9. Nani aliokoka kutoka kwa huo mji?
10. Mungu alisema ni nini itafanyika kwa mtu atakayejenga mji wa Yeriko?

Majibu

1. Yeriko.
2. Watu waliokuwa ndani walikuwa wamesikia habari ya Waisraeli kwa hivyo waliogopa.
3. Wazunguke mji.
4. Ilikuwa saba (7) kwa kila kitu.
5. Tarumbeta pekee.
6. Waliuzunguka mji mara 7
7. Wote walipiga kelele.
8. Ukuta wa mji ulianguka.
9. Rahabu na jamaa yake.
10. Atalaaniwa.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 1

20 Kuanguka kwa Yeriko

Marejeo

Yoshua 6


Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba lazima tumtii Mungu

Maneno maalum

1. Mji + Yeriko + maajabu
2. Tembea + saba + makuhani + tarumbeta + siku
3. Mara 7 + piga kelele
4. Anguka chini + angamiza
5. Rahabu + okoka + kamba nyekundu
6. Thamana + hazina ya Mungu + Mungu kwanza
7. Usijengwe + laana


20.1 Wana wa Israeli walisafiri mpaka mji wa Yeriko. Huo mji ulikuwa umefungwa na wenyeji ili wasiingie. Waliokuwa ndani walikuwa wamesikia maajabu yenye Mungu Waisraeli amewafanyia. Walikuwa na uoga wasijue la kufanya.



20.2 Mungu aliwaambia Waisraeli wauzunguke mji. Aliwaambia wafanye sawa na maagizo yake. Makuhani saba lazima wapige tarumbeta na wawaongoze kuzunguka mji. Watabeba sanduku la agano. Watafanya hivi kila


siku kwa muda wa siku saba. Watu wote watanyamaza wakati tarumbeta itakapotoa sauti.

20.3 Siku ya saba watazunguka mji tena, lakini siku hii hawakuzunguka mara moja tu, walizunguka mara saba. Baada ya kuenda mara ya saba, watu wote waliposikia tarumbeta ikilia, walipiga kelele.



20.4 Watu walipopiga kelele ukuta wa Yeriko ulianguka chini na Waisraeli waliingia ndani na kuangamiza hao watu. Mungu aliwapa Yeriko bila kupigana. Huu ulikuwa mji wa kwanza kuuchukua kwa nchi ya ahadi.

20.5 Rahabu na jamaa yake walipona. Aliweka kamba nyekundu kwa dirisha yake. Hii ilikuwa ishara yenye wapelelezi walimpa walipokuwa wakitoka Yeriko. Watu Waisraeli walipoona hiyo kamba, walijua kwamba watu wa hiyo nyumba lazima waokolewe.



20.6 Mungu aliwaambia Waisraeli wamchukulie vitu vyote vya dhamana kutoka kwa ule mji. Huu ulikuwa mji wa kwanza Waisraeli walichukuwa kutoka kwa nchi ya ahadi. Lazima wampe Mungu kila kitu cha kwanza. Hata nasi tuweke Mungu kwanza maishani mwetu.

20.7 Yeriko ilianguvizwa. Mungu alisema isijengwe tena. Alisema mtu yeyote akijaribu kujenga atalaaniwa.

Mungu alileta watu wake kwa nchi ya ahadi. Alienda mbele yao na bila kupigana aliwafungulia mji wa Yeriko na kuuchukuwa. Wakati walifanya matakwa ya Mungu, kila kitu kiliendelea vizuri.

Waliendelea kuchukuwa nchi yote ya Kanaani. Yoshua aliwaongoza maishani mwake mpaka kila kabila ya Israeli wakapewa pahali pao nchini.